

MAJLISI ZA IMAM HUSEIN (A.S)

MAJUMBANI

Kimeandikwa na:
Jamil Kamal

Kimetarjumiwa na:
Abdul Karim J. Nkusui

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:

AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 - 17 - 009 - 8

Kimeandikwa na:
Jamil Kamal

Kimetarjumiwa na:
Abdul Karim J. Nkusui

Kimehaririwa na:
Hemedi Lubumba (Abu Batul)

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Hajat Pili Rajab

Toleo la kwanza: Julai,2011
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv-com

Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info

YALIYOMO

Utagulizi.....2

Faida ya kwanza:

Ni Ulinzi katika upande wa maendeleo.....4

Faida ya Pili

Ulinzi dhi ya balaa na hatari.....9

Faida ya Tatu

Shufaa, rehema na maghfira.....13

Faida ya Nne

Funzo, utakazo na Uongofu.....21

Faida ya Tano

Kukidhi haja na kutatua Matatizo26

Faida ya Sita

Mafungamano na mapenzi ya kina.....31

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani



NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu kiitwacho, *al-Majaalis al-Husayniyyah Fi 'l-Buyuut* kilichoandikwa na Jamil Kamal. Sisi tumekiita, *Majlisi za Imam Husain AS Majumbani*.

Kila mwaka mwezi wa Muhamarram, Waislamu hususan Mashia, hukusanya-ka katika kumbi maarufu ziitwazo Husainia, Mahfil au Imambara, n.k. kuomboleza kuuawa shahidi Imam Husain AS, mjukuu wa Mtukufu Mtume SAW, katika ardhi ya Karbala (Iraq).


Katika kitabu hiki mwandishi anashauri zifanyike majlisi ndogondogo majumbani zisizo na gharama kubwa na ambazo kwa uzoefu wake ameziona kuwa zina matokeo mazuri sana.

Sisi tumeuona ushauri huu kuwa ni mzuri sana, na kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili ili wasomaji wetu, hususan Waislamu, wazungumzaji wa Kiswahili waufanyie kazi ushauri huu.

Tunamshukuru Abdul Karim J. Nkusui kwa kukubali jukumu hili la kuki-tarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa na changamoto kubwa kwa wasomaji wetu.

Mchapishaji
Al-Itrah Foundation





Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

UTANGULIZI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Rehema na amani zimwendee Kipenzi chetu Mtume Muhammad (saww) na Kizazi chake chema.

Mwandishi wa kitabu hiki kidogo kwa umbo lakini kwa hakika ni kikubwa kwa yale kilichoyabeba miongoni mwa nasaha, mafunzo na mifano chungu nzima yenye kujaa mazingatio katika maisha yetu ya kila siku na yenye manufaa hapa duniani na kesho Akhera. Mwandishi wa kitabu hiki aliniomba baada ya kukamilisha kazi ya tarjamaa pia niandike utangulizi wa kitabu hiki, nami nikaafiki hilo kwa moyo mkunjufu.

Kitabu hiki kinalenga sana kujenga maadili mema na tabia nzuri katika familia zetu na jamii yetu hususan kwa kizazi chetu ambacho ndio kwanza kinainukia na kupambana na mambo ambayo yanashughulisha akili zao na fikra zao na kuwaweka mbali na utamaduni wao na mafunzo mema ya dini yao, ambapo nafasi imekuwa ni finyu kiasi kwamba mtu hana nafasi ya kuhudhuria vizuri katika madrasa. Hivyo mwandishi wa kitabu hiki anahamasisha na kuraghribisha kuwepo majlisi ndogo katika ngazi ya familia, mtu na familia yake, jamaa zake na jirani zake na kufanya majlisi ndogo ambayo haihitaji gharama kubwa, lakini faida yake na malipo yake ni makubwa, majlisi ambazo zitalea nafsi zetu, familia zetu, jamii yetu na vizazi vyetu malezi mazuri ya kidini, lakini pia yatasaidia kujenga na kuimarisha familia zetu na nyumba zetu na kuzipa ulinzi na kinga kutokana na maafa na balaa mbalimbali na kuwa ndio sababu ya sisi kuteremshiwa baraka na rehema za Mwenyezi Mungu.

Lakini pia itakuwa ni fursa nzuri katika uwanja wa da'awa kwa kufanya tabigh ya nyumba kwa nyumba, familia kwa familia, mtaa kwa mtaa, mtu na mtu n.k. Hakika ni jambo zuri inapasa tulichukue kwa uzito mkubwa na

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

wa namna ya kipekee, na faida yake tutaifurahia hapo baadae. Tuanze nalo sasa kwa ajili ya kutengeneza mustakabali wetu na wa vizazi vyetu na tutakuwa tumevirithisha jambo zuri na lenye matunda mazuri.

Ni matarajio yetu kuwa jamii yetu hususan ya Kiafrika italipokea jambo hili zuri kwa mikono miwili na kulifanyia kazi kwani katika jamii zingine linafanyiwa kazi na tunaona matunda yake. Mwamko wao ni mzuri na wanawalea watoto wao malezi mema, la msingi ni tuhimizane juu ya jambo hili la kuhuisha majlisi hizi na tuzitumie vizuri kwa ajili ya faida yetu na vizazi vyetu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atie baraka na taufiq katika jambo hili ili jamii yetu ifaidike kutokana na matunda yake.

Wabillah taufiq

A. J. NKUSUI

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

FAIDA YA KWANZA

Ni ulinzi katika upande wa maendeleo:

Haiyumkini kupatikana umma katika umma zilizotangulia au umma uliopo katika zama hizi, unaoweza kudai kwamba unaweza kubakia kimaendeleo na kiutamaduni bila ya kuwepo dhamana tosha juu ya hilo.

Maendeleo hayawezi kubaki hai kwa kujitenga na maendeleo mengine au bila ya kuathirika na maendeleo ya watu wengine kifikra, kielimu na kiuchumi. Ni wajibu tutilie mkazo juu ya ukweli ambao watu wawili hawawezi kutofautiana juu yake, kwamba mashambulizi ya jumla ya kimagharibi sawa yawe yale ya njia ya idhaa, setelaiti na intaneti, au yale yanayosambazwa kwa njia ya runinga na mitandao mingine, yaliyobeba fikra potovu na madhara ni mengi zaidi kuliko yale yenye faida kwa jamii zetu.

Umma wowote ule ni lazima uwe na asili ya kutegemea na kumiliki nyenzo za kielimu na kiutamaduni ambazo hutoa dhamana ya ulinzi wa maendeleo ili kwamba umma usisamaratike kiutamaduni na kukabiliwa na myeyuko wa kifikra. Je tutasahau historia ya mashambulizi ya Tatari kwa Wamongolia na waliyoyafanya ikiwa ni pamoja na kuchoma maktaba na kutupia vitabu katika mto Dijilah hadi ukabadilika na kuwa na rangi ya bluu kutohana na wingi wa wino uliomwagwa humo? Je, tutasahau vita vya msalaba vya kihistoria katika nchi za Kiislamu na yale uliyoy-asababisha ikiwa ni pamoja kuleta utamaduni hatari na mabadiliko kwa Waislamu, na ambao kwa sababu yake kundi kubwa katika baadhi ya jamii katika baadhi ya nchi za Kiislam maelfu kwa maelfu bali kwa mamilioni wamebadilika na kwenda katika dini ya Kikristo?

Kwa kweli sababu ya kuanguka kwa nchi nyingi na mamlaka nyingi katika historia sio kingine bali ni kwa kukosa kinga na dhamana ya kiuta-

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

maduni na ya kimaendeleo inayoilinda dhidi ya tamaduni nyingine, kwa sababu hiyo unawaona wamemomonyoka kifikra na kitamaduni.

Majlisi za Imam Husein (a.s.) ndio dhamana, sisi tunasisitiza juu ya ukweli ulio wazi bali tunatoa changamoto kwa Ulimwengu toka kona hadi nyingine, bali kama tutatafiti katika kurasa za kihistoria juu ya taasisi ya kidini iliyohifadhi sio tu jamii yake ya Kishia bali inatoa mchango mkubwa sana katika kuhifadhi jamii ya Kiislamu isipotoshwe na kuyayuka wakati wa mapambano yake ya kimaendeleo dhidi ya jamii nyingine za zamani na za sasa, tutakuta ni ile inayoshikamana na Majlisi za Huseini (a.s.) kwa aina zake zote zinazofanywa na kundi la waumini katika muda wote wa historia hadi leo hii. Majlisi za Huseini (a.s.) ndizo zilizoleta mwamko na vuguvugu hilo la kiutamaduni na kifikra katika Umma wa Kiislamu, licha ya jamii hiyo ya Kishia kupigwa vita kwa mapambano makali, na licha ya wafuasi wake kuteswa, kuuliwa kwa makusudi na kukithiri umwagikaji wa damu zao wakati wa utawala wa dola za Bani Ummaya, Bani Abbas na nyinginezo.

Majlisi zote tunazijali na kuziheshimu, bali tanazinyenyeka kwa heshima kwa sababu yote yanayotolewa katika majlisi za Huseini si kingine ila ni mawaidha ya Kiislamu na fikra zinazohifadhi jamii kutoptu na upotovu, na kuhifadhi utukufu wa Umma. Mwenye insafu na mwenye kufuatilia majlisi hizi hataona isipokuwa mwongozo na waadhi, tukiachilia mbali kuwaelimisha watu mbali mbali kwa kiwango kinachotakiwa kiutendaji katika jamii. Hivyo majlisi hizi zimekuwa ni nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na ni mihadhara ya kutoa dira na mwelekeo sahihi wa Kiislamu usio na upotoshaji wa kihistoria, upotoshaji ambao unasifika kwa mgongano katika idadi kubwa ya kurasa zake.

Kisa kutoka Najaf tukufu:

Ananukuu Sheikh Ali Dukhail kisa hiki katika kitabu chake “*Anajafiyat*” anasema: Sheikh Ibrahim Al-Gharawiy naye alikuwa ni mmoja wa wajuzi

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

wa Najafu, ambaye alifariki mwaka 1306 A.H, alikuwa ni kimbilio la kila fakiri na hifadhi ya kila maskini, majlisi zake (alizokua akizifanya kila siku) hazikuacha kuwa ni zenye kujaa wanachuoni na watu wenye fadhila, majlisi zake zilikuwa hazikosi ukumbusho wa kielimu na matawi ya fiqh, hivyo kila mwenye mas'ala magumu au jambo asilolijua alikuwa anakua katika majlisi yake.

Nyumba za watu wenye elimu Najaf zilikuwa katika mfano huu (Haya tumeyashuhudia) bali hata majlisi za watu wa kawaida pia zilikuwa hivyo; achilia mbali misikiti na sehemu takatifu, utasikia sauti za wanachuoni katika waadhi wa alasiri hata ukiwa nje ya uzio.¹

Maelezo:

Kama majlisi zetu zitakuwa za aina hii na kwa mfano huu mzuri, je, hatuna haki ya kujifikharisha na majlisi za Imam Husein (as) na kutilia mkazo kwamba zilikuwa na bado zingali zinahifadhi ustaarabu na maendeleo ya Kiislamu dhidi ya upotofu.

Fadhila za majlisi za Imam Husein katika kueneza Uislam katika kiji-jji kimoja huko Afrika:

Ayatullah Al- Udhmaa Marjaa wa dini As-Sayyid Muhammad Shiraziyy (r.h) anasema: Alinijia mmoja wa waumini kutoka Afrika jina lake ni (Hajj Swafar Sharyni Duyujiy) na alikuwa ni mkarimu, mwenye kuheshimika na mwenye umaarufu akasema: 'Hakika mimi huwa nakwenda katika baadhi ya vijiji vya Kiafrika kila mwaka na huchagua kijiji kisichokuwa na kiongozi wa kidini ili nikasome majlisi kwa muda wa siku kumi za Muharram bila ya malipo yoyote.

¹ *Ma'arifu Rijal* Juz: 1 Uk: 30

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Siku moja niliwasili katika kijiji nikauliza watu wake: Je, mna kiongozi yeoyote wa dini au khatibu? Wakasema: Hapana. Nikasema: Je, mnasoma majlisi ya Husein? Wakasema: Ndio. Nikasema: Je, mnataka niwasomee majlisi katika mwaka huu? Wakasema: Ndio, karibu. Wakanichukua hadi kwenye nyumba kubwa na ilikuwa imepambwa kwa nguo nyeusi na alama za maombolezo zimening'inizwa katika kuta kama tunavyofanya sisi Shia katika sehemu mbalimbali, niliwasili kwao kabla ya kuingia mwezi wa Muhamarramu kwa siku moja, lakini ulipowadia wakati wa swala ya Adhuhuri sikusikia sauti ya adhana. Nikawauliza: Kwa nini hamtoi adhana kwa ajili ya swala? Wakasema: Swala ni nini? Nikawaeleza maana ya adhana. Wakanyamaza na hawakuelewa maneno yangu. Nikawauliza: Msikiti uko wapi? Wakasema: Msikiti ni nini? Nikamuuliza mmoja wao: Nini dini ya watu wa kijiji hiki? Akasema: Hakika wao ni wapagani. Nikasema wote? Akasema: Ndio. Nikasema hapa hakuna dini ya kiislamu? Akasema Uislamu ni nini? Sisi hatujui maana ya Uislamu. Nikapanda juu ya mimbari nikawa nawaeleza juu ya itikadi na maana ya Uislamu hadi mwisho wa siku kumi, basi wakabadilika wote na kuwa Waislamu na wakawa mionganoni mwa wafuasi wa Imam Ali bin Abi Twalib kwa baraka za majlisi za Imam Husein katika nyumba ya mmoja wao.

Al -Imamu Shirazi na kuhamasisha majlisi za Imamu Husein (as):

Amenisimulia mmoja wa waumini wa kweli ambao wamefanya kazi pamoja na Ayatullah As-Sayid Shiraziy (r.h) wa Kuwait kuhusu harakati za kasi na makini za Imam Shiraziy (r.h) kwa ajili ya kuhifadhi kadhia ya Husein (as) yenye vuguvugu na harakati hususan unapowadia mwezi wa Muhamarram. Anasema: Imam Shiraziy (r.h) alikuwa anahamasisha harakati kama ilivyo ada yake, katika mwezi wa Muhamarram anatoa maelekezo ya kuunda kamati kwa ajili ya maadhimisho ya maombolezo ya Imam Husein hususan kushajiisha maadhimisho haya katika majlisi za Imam Husein za majumbani kwa utaratibu ufuatao:-

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Kugawa vitambaa maalum vyenye nembo na alama ya mapinduzi matukufu ya Imam Husein .

Kugawa vitabu na makala yanayohusiana na majlisi hizo za nyumbani.

Kuhuisha majlisi za nyumbani katika sehemu za vijijini na zisizozoleka, mfano kuasiisi majlisi za Huseini (a.s.) katika sehemu za kuoshea maiti katika sehemu za Mashariki* ndani ya msikiti mdogo, na msomaji alikuwa ni Sayid Mahdiy Al-Handawiy, naye ni shahidi juu ya hilo.

Kuhimiza na kuhamasisha wengi wa waumini kuhudhuria ambapo alikuwa anachukua jamaa na shakhsiyati, nao wanazunguka pamoja naye katika majlisi zile licha ya wingi wa kazi zake, hiyo ni ili kushajiisha mahudhurio katika majlisi hizo, ambapo mmoja wa waumini anaeleza kuwa tunapotoka tu katika majlisi ya Huseini (a.s.) tunayoifanya katika moja ya nyumba ya mmoja wetu huingia moja kwa moja katika nyumba inayofuata ili kuhudhuria majlisi nyingine, vivyo hivyo hadi usiku wa manane.

Kutoa kwake Mawaiida maalum kwa makhatibu na kuwaelekeza aina za mawaiida na fikra ambazo zinapasa kutolewa katika mfano wa majlisi hizo ili zitolewe kwa wingi na katika sura bora zaidi.

Na alikuwa na harakati nyingi za kielimu katika nyanja hii ambazo zilikuwa na athari katika kubadili watu na familia nyingi na kuwa watu wenye kushikamana na dini na mafunzo ya Kiislam kwa baraka za majlisi hizo tukufu.

* Ni moja ya sehemu katika mji wa Kuwait

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

FAIDA YA PILI

Ulinzi dhidi ya balaa na hatari:

Tabia ya nafsi ya mwanadamu kwa kawaida haipendi machungu na mavimivu, sawa yawe ya kinafsi au ya kimwili. Ni nani kati yetu asiyependa kuwa mbali na maradhi, balaa na matatizo ya kiafya au ya kinafsi katika zama ambazo wenye afya nzuri ni wachache mno? Maafa na balaa ni moja ya mishale ya kudura iliyoelekezwa kwetu, kila mmoja kwa kiasi alichokadirwa, lakini aliyeleta ugonjwa pia ameleta dawa na mambo yanabadijika kwa kudura ya Mwenyezi Mungu na elimu Yake ya awali, ya sasa na ya baadaye, ametukuka Muumba. Kwani riwaya zenyenkuaminika Mfano: “Hukumu haitenguliwi ila kwa dua” na “Zuieni balaa kwa kutoa sadaka” na “Sadaka inakinga vifo vibaya sabini,” hizi zote zinatilia mkazo kwamba amali ya kheri si kingine bali ni ngao inayomkinga mwanadamu kutokana na mashambulizi ya balaa na maafa.

Na kati ya aina za dawa zenyenkuamini kufaulu sana katika kuzuia misiba na balaa ni majlisi za Imam Huseni (as), hivyo ni bora kwa waumini kutoa kipaumbele kwa kuimarisha na kuzingatia mfano wa majlisi hizi katika nyumba zao ili wapate ulinzi na uangalizi wa Mwenyezi Mungu na karlama za Imam Huseni (as) na kukingwa na balaa zilizokwishahukumiwa. Kwani Mwenyezi Mungu amekataa mambo kwenda isipokuwa kuitia katika sababu zake. Ni mara ngapi majlisi hizi zimezuia madhara ya balaa na fitina, na zikarejesha upepo mbaya wa maradhi na mauti kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na kwa baraka za majlisi hizi tukufu zinazopendeza mbele ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya bwana wa vijana wa Peponi?

Kama ambavyo kuna kanuni za mbinguni za ghaibu kwa ajili ya kuteremsha balaa vile vile Mwenyezi Mungu amejaalia kwa upande mwingine sababu na zana za kuzizua na kuzirejesha, kwani ni vibaya kwa

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Muumba kutuletea balaa kwa hoja ya kutahiniwa na kujaribiwa bila ya kutoa mbinu za kujikinga na kujihadhi, aliyetoa uwezo wa kuponya kwa vidonge vya dawa ameyapa majlisi ya Imam Husein zaidi ya hayo.

Tunaeleza baadhi ya mifano tu katika njia ya kutoa mfano na wala si yote, kuhusiana na faida za majlisi hizo katika kukinga, na kwamba ndio kinga katika dunia na Akhera:

Kisa cha Al-Haji Mujibil:

Iraqi ni kama nchi zingine za Ulimwengu - tangu miaka mingi – ilikuwa inakabiliwa na maradhi na balaa, sawa iwe ni kipindupindu, tauni, taifodi na mfano wa hayo kati ya maradhi ya mlipuko yanayoenea haraka, na wengi walikuwa wakidhurika na hata wakati mwengine baadhi ya nyumba zilibaki tupu. Na ili kuyatokomeza maradhi hayo walikuwa wanataswasali kwa Mwenyezi Mungu kwa kufanya majlisi za Abu Abdillahi Al-Huseini (as) katika mitaa, vichochoro, barabarani na majumbani.

Ananukuu Al-Haji Mujibil* kisa cha kabla ya miaka arobaini takriban, anasema: "Tulikuwa tumefanya majlisi za maombolezo ya Imam Husein (as) katika uwanja wa Dhay'ah – yaani majlisi maalumu ya ndani - pindi balaa iliposhuka Iraqi, na baada ya kumalizika majlisi nililala katika sehemu tuliyofanyia majlisi, usingizini niliona watu watatu wenye silaha mmoja wao alinilenga, lakini swahiba zake wakamkataza na wakamwambia: Tazama athari za majlisi za Husein, hili tandiko bado lingali limetandikwa na hii meza juu yake yanawekwa mabirika ya chai na kahawa, nenda katika sehemu nyingine. Anasema: Asubuhi zikapelekwa

* Naye ni muuza vitambaa Najaf kati ya watu wema na ametoka katika kiunga cha Ramiyah (Iraq) Na alifariki mwaka 1373 A.H katika mji wa Najaf .

² *Najafiyaat* Uk: 146.

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

sanda tatu kwa watu wa sehemu hiyo.”²

Hakika ni muujiza wa Imamu Husein (as):

Amesema Marja'a mashuhuri Ayatallahi Al-Udhma As-Sayid Al-Burjurdii (r.h): “Nilipokuwa Burjurdii (Iran), nilikuwa nasumbuliwa na maumivu makali sana katika jicho, nilikwenda kwa matabibu, lakini walikata tamaa kwa matibabu yangu. Katika siku za Ashura msafara wa maandamano ya maombolezo ulikuwa na ada ya kuja nyumbani kwetu (kuja kufanya majlisi ya Imam Husein katika nyumba yake), hivyo nilikaa nikilia katika majilisi ya Husein na jicho lilikuwa linaniuma sana, wakati nikiwa katika hali hiyo ikanijia akilini mwangu hisia ya kupangusa vumbi ambalo lilikuwa katika nyuso na miili ya waombolezaji na kupaka kwalo jicho langu huenda litapona. Nilifanya hivyo bila yeoyote kutambua hilo, punde tu nilipofuta kwalo jicho langu nikahisi nafuu ya maumivu, na jicho langu likaanza kupona pole pole hadi maumivu yote yakaondoka kabisa, na hayajarejea hadi leo hii, bali nimekuwa naona kwa uzuri zaidi bila ya kuhitajia miwani.”

Na ajabu ni kwamba marhum Al-Burjurd (r.h) alipofikia umri wa miaka themanini na tisa baadhi ya matabibu bingwa walichunguza jicho laje lakinii hawakukuta udhaifu wa aina yeoyote hadi wakasema: Hakika utalaamu wa kitabibu unahukumu kuwepo na udhaifu katika jicho la binadamu katika umri huu, sasa itakuwaje kwa mwanadamu ambaye amelichosha kwa kusoma kwa muda wa miaka mingi na alikuwa anasumbuliwa na udhaifu na maumivu ya jicho lake awali? Hakika si kingine ila ni muujiza wa Husein (as).³

Na maelezo yaliyotangulia yanatiwa mkazo na riwaya sahihi kutoka kwa Abu Bakri Al-Hadharamiy kutoka kwa Abu Abdillah As-Sadiq (as) amese-

³ *Bandahay Jawidan cha (Kifurusi) Uk: 61*

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

ma: "Lau kama mgonjwa kati ya waumini angejua haki ya Abu Abdillah (as), utukufu wake na uongozi wake, angechukua udongo wa kaburi lake kwa mapenzi na mahaba na ingekuwa ni dawa na ponyo kwake."⁴

Majlisi na ziara ya Ashura na athari zake za ajabu:

Amesema muasisi wa Hawza ya Qum tukufu Ayatullah Al-Udhamaa Sheikh Abdul-Karim al-Hairiy (r.a.): "Tulikuwa tumekaa kwa Ayatullah Al-Udhamaa Al-Mujadid Ashirazy huko Samara, ghafla akaingia Ayatullah As-Sayid Muhammad Al-Fasharikiy huku uso wake ukiwa ume-jaa huzuni na inadhihiri kwamba alikuwa amechoka kutokana na maradhi ambayo yalikuwa yameikumba Iraqi siku hizo. Mwalimu wetu Ayatullah Ashiraziy akatuambia: Je, mnionna kuwa ni mujtahidi au laa? Tukasema: Ndio tunakuona kuwa ni mujtahidi. Akasema: Je, mnionna kuwa ni mwadilifu? Tukasema: Ndio. Na Mujadid alikuwa anataka kwa maswali haya mawili kuchukua kwa wanafunzi wake kiapo ili atoe hukumu ambayo hawatosita katika kuitekeleza.

Hivyo tulipokiri juu ya ijtihami yake na uadilifu wake, akasema: "Hakika mimi namwamuru kila mwanamke na mwanaume kati ya Mashia asome ziara ya Ashura kwa niaba ya Mzazi Mtukufu wa Imam Al-Hujjah (as) na watawasali kwa mtoto wake (as) ili atuondolee balaa." Baada ya hapo yal-ifanywa majlisi maalumu kwa ajili ya ziara ya Imam Husein katika kila nyumba na kukawa na majlisi za Huseini (a.s.) katika kila nyumba.

Anasema Ayatullah Al-Hairy: "Kwa kutolewa tu hukumu hii, Shia wa Samara wakajilazimisha kutii, na matokeo yalikuwa ni kwamba hakuna ye yote aliyefariki kwa maradhi haya kati yao, wakati ambapo kwa siku moja walikuwa wanakufa watu kumi hadi kumi na tano kwa wasiokuwa Shia, kwa sababu ya maradhi haya."⁵

⁴ Kamiluz-Ziyraat Uk: 467

⁵ Ziyaratul Ashuraa wa Athaaruha al- Ajiybah: 41

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Kutoka kwa Hisham bin Al-Hikam kutoka kwa Fadhiyli bin Yasir amesema: Amesema Abu Abdillahi As-Sadiq (as): “Hakika karibu yenu kuna kaburi – yaani kaburi la Imam Husein (as) - hajaliendea yejote mwenye shida ila Mwenyezi Mungu amemuondolea matatizo yake na kumkidhia haja yake.”⁶

FAIDA YA TATU

Shufaa, rehema na Maghfira:

Kama hisia zitatuchukua na kutuzungusha na tukajikuta katika Siku ya Kiyama katika kile kisimamo ambacho kinatisha, ambapo zinatuzunguka hatari za kuogofya kila sehemu kama isemavyo Qur’ani tukufu, ambapo siku moja:

﴿ فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ حَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ ﴾

“Katika siku ambapo muda wake ni sawa na miaka hamsini elfu.” (Surat al-Maarij: 4).

﴿ فَإِذَا الْنُّجُومُ طُمِسَتْ ﴿١﴾ وَإِذَا الْسَّمَاءُ فُرَجَتْ ﴿٢﴾ وَإِذَا الْجِبَالُ نُسِفَتْ ﴿٣﴾

“Nyota zitakapofutwa (nuru yake), mbingu zitakapopasuliwa na milima itakaposagwasawa. (Sura Mursalat: 8 – 10).

﴿ إِذَا الشَّمْسُ كُوَرَتْ ﴿٤﴾ وَإِذَا النُّجُومُ أَنْكَدَرَتْ ﴿٥﴾ وَإِذَا الْجِبَالُ سُرِّئَتْ ﴿٦﴾

﴿ وَإِذَا الْعِشَارُ عُطْلَتْ ﴿٧﴾ وَإِذَا الْوُحُوشُ حُشِّرَتْ ﴿٨﴾ وَإِذَا الْبَحَارُ سُجَّرَتْ ﴿٩﴾

“Na jua litakapokunjwa kunjwa na nyota zitakapoanguka na milima itakapopeperushwa na ngamia wenyewe mimba watakapoachwa, na wanyama watakapokusanya na bahari zitakapowashwa moto.” (Sura Takuwir: 1 – 6).

⁶ Kamiluz-Ziyaraat Uk: 312.

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Na kuhusu baadhi ya aina za adhabu kwa wenyewe madhambi anasema (swt):

﴿ وُجُوهٌ يَوْمَئِنْ خَشِعَةٌ ﴾ عَامَلَةٌ نَّاصِبَةٌ ﴿ تَصْلَى نَارًا حَامِيَةً ﴾
 ﴿ تُسْقَى مِنْ عَيْنٍ إِانِيَةً ﴾ لَيْسَ لَهُمْ طَعَامٌ إِلَّا مِنْ ضَرِيعٍ ﴾ لَا
 يُسْمِنُ وَلَا يُغْنِي مِنْ جُوعٍ ﴾ ﴿ يَوْمٌ يَكُونُ النَّاسُ كَالْفَرَاشِ الْمَبْثُوثِ ﴾ وَتَكُونُ الْجَهَالُ كَالْعَهْنِ الْمَنْفُوشِ ﴾

“Nyuso siku hiyo zitakuwa na huzuni, zitatumika na kutaabika, zitain-gia katika moto mkali, zitanyweshwa katika chemchem iwakayo, hawatakuwa na chakula isipokuwa cha miba, hakinenepeshi wala hakiondoi njaa.” (Sura Ghashiya: 1 – 7).

Na katika kuelezea kutapaka mamilioni ya watu katika uwanja wa Kiyama anasema Mola Mtukufu:

﴿ يَوْمَ يَكُونُ النَّاسُ كَالْفَرَاشِ الْمَبْثُوثِ ﴾ وَتَكُونُ الْجَهَالُ كَالْعَهْنِ الْمَنْفُوشِ ﴾

“Siku watu watakapokuwa kama panzi waliotawanywa na milima itakapokuwa kama sufi iliyochambuliwa.” (Sura al-Qaria’ah: 4 – 5).

Na utakatika uhusiano wote wa kijamii na kibinadamu hivyo uhusiano hautanufaisha katika siku hiyo:

﴿ يَوْمَ يَفْرُّ الْمَرءُ مِنْ أَخِيهِ ﴾ وَأُمِّهِ وَأَبِيهِ ﴾ وَصَاحِبِهِ وَبَنِيهِ ﴾
 لِكُلِّ أَمْرٍ يِمْنُهُمْ يَوْمَئِنْ شَانٌ يُغْنِيهِ ﴾

“Siku mtu atamkimbia ndugu yake, mama yake, baba yake, mke wake, na watoto wake, kila mtu kati yao siku hiyo atakuwa na jambo linalomtosheleza yeze tu.” (Sura Abbas: 34 – 37).

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Lakini ni kipi kitakachomnufaisha katika wakati huo mgumu, wakati utakapokatika uhusiano wa aina zote, kuwakimbia vipedzi na kujuta kwa mwanadamu: **“Anasema: Laiti ningetanguliza kheri kwa ajili ya maisha yangu.” (Sura al-Fajri: 24).**

Ndio, hakika ni Shufaa (uombezi) wa Husein (as) na babu yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Ahlul – Bait (as).

Lakini kwa nini iwe ni Husein (as) ?

Hakika Husein (a.s.) na wafuasi wake walipata mauaji mabaya mno katika historia kwa kongamano la waandishi wote, na ametoa muhanga ambao hajautoa yejote kabla yake wala baada yake. Na hajafanya ubakhili kwa chochote, katika njia ya Mwenyezi Mungu, katoa watoto wake hadi mtoto wake mchanga. Je Mwenyezi Mungu atamnyima wasila wa Shufaa kwa wanaopenda na kumfuata katika upande wa kumpa badili na malipo? Je tunamtengea bwana wa mashahidi walau nusu saa kila wiki kwa kufanya majlisi ya Huseini (a.s.) katika nyumba zetu, kwa kuwakusanya humo jamaa, ndugu na marafiki? Je, ndani ya mwaka mzima tunafanya majlisi za Maimamu katika minasaba mbalimbali?

Kuna familia nyingi ambazo zimepata taufiq kwamba nyumba zao hazikosi kufanya majlisi za Imamu Husein (a.s.), kulisha chakula na mengine mengi mionganoni mwa harakati, kwa jina la Bwana wa Mashahidi, hakika hawa wana uombezi kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na watae-pushwa na moto Siku ya Kiyama.

Madhumuni ya kutaja haya ni kwamba wale wote walioanzisha majlisi hizo katika nyumba zao uamuzi wao huu haukuja bure bali ni kwa kuwa wao wamepata taufiq na uanganizzi kutoka kwa bwana wa mashahidi, kwa kuwa majlisi hizi zina athari nzuri duniani na Akhera.

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Kisa cha Sayid Dar'weshi:

Ameandika marhumu mwanachuoni mtukufu na mwema Sayid Muhammad, Swadiq Al-Hakim mtoto wa Ami yake Ayatullah Al-Udhma Sayid Muhsin Al-Hakim (r.a) kwamba: Najafu kulikuwa na uchochoro unaoitwa *Twaq Sayid Ali Dar'wesh*, humo aliihi mwanaume fakiri kati ya madar'wesh, jina lake ni Sayid Ali, na kiasi fulani alikuwa anaudhi watu na hakuna yejote aliyejkuwa anapita katika uchochoro huo kwa kujiepusha naye. Siku moja mmoja wa makhatibu wa Najafu alipitia katika uchochoro huo katika siku za kumi la mwanzo la mwezi wa Muharram akiwa na haraka, na kupita kwake ilikuwa ni katika usiku wa siku ya kumi ya Muharram, Sayid Ali Dar'wesh akamzuia njiani na akamwambia unakwenda wapi kwa haraka hivi?

Khatibu akasema: "Nina majlisi na nataka kufika haraka." Sayid Ali Dar'wesh akasema: "Njoo hapa na unisomee majlisi kwa muhtasari na nielezee msiba wa Imamu Husein (as.)." Akasema: "Sayid Ali niruhusu niende kwenye majlisi yangu na wala usinifanyie mzaha." Akamwambia: "Mimi sitanii, tafadhali nisomee majlisi na ueleze humo msiba wa Imam Husein (as.)." Khatib akasema: "Nitamsomea nani maombolezo na wala hakuna yejote, vile vile sisi makhatibu hatusomi bila ya kuwepo na mimbari." Kwa mshangao akainama ardhini kwa mikono yake na miguu yake kwa namna ambayo mikono yake na miguu yake ikawa kama mfano wa nguzo za mimbari na akaniambia kaa hii ni mimbari na nisomee majlisi ya maombolezo.

Khatibu anasema: Nilikuwa na haraka nataka niachane na huyu Dar'wesh nikaonelea ni bora nikae na nisomee msiba wa Imam. Nikakaa juu ya mgonogo wake nikasema: "Asalam alayka yaa Aba Abdillahi Al-Husein, asalam alayka ya madhlum ya Husein." Hapo nikasikia sauti ya Sayid Ali Dar'wesh, akilia na akapaza sauti kwa manjonzi na kilio. Baada ya hapo nikamuomba ruhusa na nikamuaga na nikaondoka haraka.

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Siku tatu baada ya Ashura nilimuona mmoja wa watukufu akanipa habari za kufariki kwa Sayid Dar'wesh. Nikasema: "Al-hamdulillahi ambaye amewapumzisha watu na shari yake." Mtukufu huyo akaniambia: "Nimeona katika usingizi wangu kwamba amesamehewa dhambi zake." Nikamwambia vipi? Akasema: "Niliona katika ndoto kwamba mimi niliingia katika eneo la kaburi la Amirul-Mu'minina (as) na Imam amesimama uwanjani, hapo watu walikuja na jeneza la Sayid Dar'weh wanataka wamzike humo, Imam Ali (as) hakuwaruhusu kwa hilo. Hivyo wakataka kutoa jeneza, na ndipo ghafla nikamuona Imamu Husein (as) ameingia katika uwanja kwa haraka na akasimama karibu na baba yake (as) na akasema: "Ewe baba yangu niruhusu mimi nimzike maiti huyu hapa." Amirul-Muuminina (as) akasema: "Ewe mwanangu inapasa usizike maiti hii hapa." Hapo nikaona Imamu Husein (as) anasoga hatua karibu na baba yake na akasema: "Ewe baba yangu je inajuzu kuchoma mimbari yangu?" Nikaona Imam Ali (as) ametokwa na machozi kutoka machoni mwake na akasema: "Hapana ewe mtoto wangu haijuzu kuchoma mimbari yako." Imam Ali akaamuru kurejeshwa jeneza la Sayid Dar'wesh, na mimi siku-fahamu Imam anamaanisha nini asemapo mimbari? Nikauliza hii ni maiti ya nani? Wakaniambia ni ya Sayid Dar'wesh."

Khatibu akalia kwa huzuni sana aliposikia kisa hiki, na akasema ndoto hii ni ya kweli na maudhui ya mimbari ni sahihi vilevile. Na kwamba huyu Dar'wesh alikuwa ni mimbari yangu siku ya kumi ya mwezi wa Muhamarram, nilikaa juu yake na nikasoma msiba wa Abu Abdillahi Al-Husein (as).⁷

Maelezo:

Ikiwa kitendo cha huyu mtu wa kawaida ambaye alijitolea, tena siku moja tu kuwa mimbari ya Husein (as) amepata shufaa, sasa itakuwaje kwa wafuasi, wapenzi na watetezi wa Husein (as) wanaofanya majlisi za Imamu Husein na wanaojitahidi kuthibitisha mapenzi yao kwa Ahlul-Bait

⁷ Jazaal -A'amal: 55

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

(as), unadhani Husein atatusahau katika shufaa yake siku ya Kiyama? Hapana, hapana. Amesema kweli Imam Ali bin Al-Husein (a.s.) pale ali-posema: “Muumini yejote ambaye jicho lake litalia na kudondosha chozi moja tu kwa ajili ya kuuliwa Husein bin Ali (as) hadi likatiririka katika shavu lake, Mwenyezi Mungu atampa makazi peponi, humo atakaa miongo mingi.”⁸

Kisa cha Marhum Sayid Mirza:

Sayid Mirza, Ja’far bin Sayid Al-Mirza Habibullah as-Shiraziy mtoto wa Ami yake Al-Mujadid As-Shiraziy Ayatullah Muhammad Husein As-Shiraziy (r.h), na ndugu wa Ayatullah Al-Udhma Al-Mirza Mahdiy Shiraziy Al-Hairy (r.h), mzazi wa Al-Marja’ a al-A’alaa Sayid Muhammad Shiraziy (r.h), ambaye ni mionganoni mwa maulamaa wajuzi katika nchi ya Iraqi, Marhum huyo anesema:

“Siku moja nilikwenda kwenye nyumba ya Al-Marhum Al-Mirza Abdul-Hady Ashiraziy (r.h), naye akaniambia: ‘Ewe Mirza nisomee majlisi ya Husein.’ Akanikazania juu ya hilo, nikasema nisamehe kwa hilo mimi sio khatibu, akasisitiza na akaniambia: ‘Jana nimemuona katika ulimwengu wa ndoto Imam Abu Abdillah Husein (as) na pembezoni mwake akiwa na mtoto wake, na mkononi mwake kulikuwa na orodha ya majina ya makhatibu. Imam akamwambia mwanae (as) andika jina la Mirza Ja’far Shiraziry katika orodha hii.’ Mirza Ja’far akasema: Niliposikia ndoto hii nikalia na nikasema: Jana nilikusanya familia yangu na nikawosomea msiba wa Imam Husein kutoka katika kitabu wakalia na nikalia (huenda Imam amenijumuisha katika shufaa kwa kuanzisha majlisi hii ya nyumbani). Akaongeza: Nikamwambia Mirza Abdul-Hadiy: Nimesikia na kutii na nikaanza kusoma majlisi tangu siku hiyo.”

⁸ Kamiluz- Ziyaraat: 201

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Marhum Sayid Mirza Ja'far hakuacha kusoma majlisi hadi alipofariki mwaka 1370 A.H, na amezikwa katika mji wa Rai katika makaburi ya Abul-Futuh Ar Raziy.⁹

Kutoka kwa Swalehe al-Uqbah kutoka kwa Abu Abdillah as-Sadiq (as) amesema: "Mwenye kusoma ubeti mmoja wa maombolezo ya Imam Husein akalia na kuwaliza watu kumi, atapata Pepo na wao pia watapata Pepo." Imam aliendelea hadi aliposema: "Mwenye kusoma ubeti wa maombolezo ya Imam Husein akalia au akajaribu kuwaliza basi atapata Pepo."¹⁰

Mwanamke aliyejikuwa anafanya majlisi za Huseini (a.s) aeneza rehemma makaburini:

Kutokana na uraghibishaji na uhamasishaji wa Al-Marja'a al-A'alaa Al-Imam Sayid Muhammad Shiraziy, dada mmoja kati ya waumini wanawake wa Kuwait, naye ni Al-Hajati Ummu Mahdiy (Nasiymah Ibrahim Al-Hadad (r.h)) alianzisha majlisi ya Huseini katika nyumba yake ambayo ilikuwa ni nyumba ya kawaida tu, katika moja ya vitongoji vya Kuwait.*

Alifunga azma ya kufanya majlisi za Huseini kwa kusukumwa na mapenzi yake kwa Bibi Fatma (as). Na alifanikisha hilo kwa kusaidiana na kundi jingine la waumini wanawake. Majlisi ilikuwa ni changamfu na yenye harakati kwa kufanya minasaba mbalimbali ya mazazi, maombolezo na miadhara. Mahudhurio yakawa yanaongezeka na kuwa makubwa siku baada ya siku na yakapewa jina la *Huseiniyatul-Haurau* (as).

Ila kudura haikukosea wala haitokosea shabaha yake na haikumpa Al-Hajat Ummu Mahdiy fursa ndefu ya kuishi, ambapo alifariki na kwenda kwa Mola wake tarehe 31/10/1995 akiwa na umri wa miaka ishirini na saba kwa maradhi aliyyopata baada ya kujifungua kwa siku chache, na akaen-

⁹ *Mardan Dari Maidanamai 1* cha Kifursi.

¹⁰ *Al- Biharul- Anwar* Juz: 44 Uk: 289

* Nayu ni sehemu ya Sal'wa katika mji mkuu wa Kuwait

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

da kwenye makazi yake ya Akhera akifuatiwa na amali yake njema na shufaa ya Zahraa (as) na Husein (as), na alifanyiwa maandalizi ya mazishi na kuzikwa katika makaburi ya al-Ja'afariyah katika moja ya sehemu za Kuwait.

Lakini baada ya kuzikwa siku chache baadae mume wake alinipigia simu naye ni mmoja wa waumini na akanipa habari kwa tukio hili, kwamba mwanamke aliwapigia simu na akawapa habari kwamba yeye ameona ndoto ya ajabu, kwamba mmoja wa jamaa zake wa karibu aliyezikwa katika makaburi hayo amemjia katika ndoto na akamwambia kuwa tulikuwa katika dhiki ya kutisha kwa muda mrefu, (huenda yeye hakuwa kati ya watu wenye kufanya kheri), lakini kabla ya siku chache baada tu ya kuzikwa karibu yetu mwanamke, ilinipata hali ya furaha na sururi mimi na wale wa makaburi ya jirani, tukaondolewa dhiki na huzuni na ikaja mahala pake faraja na raha.

Mwanamke akaongezea: Tulikwenda ili kuhakiki ndoto hiyo na mwanamke ambaye hatukujua chochote juu yake kabla ya hapo, tukakuta ni sahihi na kwamba yule mwanamke aliyezikwa karibu na kaburi la jamaa yetu ni Al-Hajat Nasimah Ibrahim Al-Hadad (r.h) mwenye kufanya majlisi ya Huseini.

Na tukio hili lilienea kwa mapana na mrefu kwa jamaa na marafiki na majlisi ya Huseini yangali yanaendelea hadi leo hii, na yamehamishiwa kwenye nyumba ya mmoja wa waumini katika sehemu nyingine kwa lengo la kuyaboresha zaidi na ili yachukue wahudhuriaji wengi zaidi. Pongezi kwa mwenye kuunganishwa na safina ya Huseni (as).

Ayatullah Al-Udhamaa Gul-Payganiy na kuomba kwake shufaa ya Husein (as):

Ayatullah Al-Udhamaa Gul-Payganiy (r.h) alikuwa na mapenzi makubwa sana na Imam Husein (as), alikuwa anawakusanya jamaa zake na watoto

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

wake siku ya Ashura katika nyumba yake na yeye mwenyewe anawasomea msiba wa Imam Husein (as) na yale yaliyomsibu yeye, familia yake na wafiasi wake katika ardhi ya Karbala. Na alikuwa anasema: “Kwa haya nataka Mola wangu anisajili kama mmoja wa wapenzi wa Imam Husein (a.s.) na kati ya makhatibu wenye kutaja msiba wake.”

FAIDA YA NNE

Funzo, utakaso na uongofu:

Amesema Mwenyezi Mungu (swt): “**Yeye ndiye aliyempeleka Mtume katika watu wasiojua kusoma naye akiwasomea Aya Zake na ali-watakasa na akiwafunza kitabu na hekima.**” (Sura al-Jum’ah: 2).

Hakika kazi ya kutakasa nafsi kutokana na makosa na maradhi ya nafsi, kama vile chuki, husuda, ria, ubakhili, kusengenya n.k, ndio kusudi na lengo la awali la kuletwa Manabii (as), ama lengo jingine la pili lenye kukamilisha jukumu la Manabii (a.s.) ni katika upande wa kufundisha, kuelimisha mafunzo ya kweli ya mbiguni kwa ajili ya masilahi ya mwanadamu.

Nabii wetu Mtukufu (saww) kufuatana na Aya tukufu iliyotangulia amekuja kuimarisha misingi hii miwili: Kutakasa na kuelimisha, kwa sababu hivyo ndio vipenyo viwili visivytengana. Kisha ikaja nafasi ya Maimamu wa Ahlul-Bait (as) ili kukamilisha sira hii na kuihifadhi kutokana na upotoshaji, na Imam Husein (as) alikuwa na nafasi ya kiungo katika kuidhibiti dini ya babu yake (saww), na majlisi hizi zilizoenea kila kona ya ulimwengu si kingine isipokuwa ni vituo hai vinavyobubujika elimu, utamaduni,

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

malezi na mafundisho.

Tofauti baina yetu na baina yao:

Watoto wetu kwa miaka mingi pamoja na kuchanganyikana kwao na utamaduni na fikra zingine ila sisi tunawaona wamejipamba na fikra za Ahlul-Bait (as) na itikadi yao bila ya kuathiriwa na fikra zingine au na wale wanao wanyemelea. Mwenye kuangalia vizuri ataona kuna tofauti kubwa baina ya mwenye kuhudhuria na kudumu katika majlisi za Imam Husein (as), sawa awe mdogo au mkubwa, na baina ya yale makundi mengine yaliyo mbali na mazingira haya; kwani miaka yote utawakuta vijana wa Husein (as) wengi wao wanamiliki mtazamo na maalumati mengi ya dini yao na wanajua sharia kwa kiasi kikubwa kutokana na kuathirika kwao na yale yanayotolewa na makhatibu wa mimbari ya Husein (a.s.) katika upande wa kutakasa, kuelimisha, na katika mifano ya utendaji na ufuataji wa sira na maisha ya Mtukufu Mtume (saww) na Maimam watukufu.

Ni wangapi wasiokuwa sisi wanaotamani manufaa haya? Hivyo, hakika ni neema kati ya neema za Mwenyezi Mungu kwetu. Inapasa kwa waumini – Mwenyezi Mungu awahifadhi - kufanya majilisi hizi kwa wingi kwa kuwakusanya jamaa wa karibu, familia hata kwa wiki mara moja.

Viongozi wetu wakiwemo Marja'a wakubwa na Maulamaa wetu wanajituma kwa msisitizo mkubwa kufanya majlisi hizi katika nyumba zao pamoja na kwamba wao wanaishi katika mazingira ya kusoma na kufundisha pamoja na watoto wao, ni kwa sababu majlisi hizi ni moja kati ya sifa nzuri kwetu, na haya ndio tutakayoyafafanua katika visa vifuatavyo:-

Kujifunza khutuba katika majlisi za Imam Husein (as):

Sheikhe Al-Waith Abdul-Husein Al-Khurasaniy (Mwenyezi Mungu amhifadhi) kutoka kwa baba yake Sheikh Muhammad Ali Al-Khurasaniy (r.h) anasema: "Nilipokuwa mdogo, baba yangu alikuwa ananichukua na

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

kunipeleka kwenye majlisi za kidini, anasoma na kutoa waadhi katika mimbari hadi anapofika katika kusoma maombolezo ya Imam Husein, hapo ananitaka mimi nikamilishe majlisi kwa kusoma beti za maombolezo ya masaibu ya Ahlul-Bait (as), ananiita akiwa juu ya mimbari: Soma ewe Abdul-Husein. Na alikuwa ananiambia jihadhari na kusema uongo kwa ajili ya kuwaliza watu, alikuwa anasema ipe mawaidha nafsi yako kwanza kisha ndipo uwape watu mawaidha na wala usipande mimbari kwa ajili ya kupata mali.”¹¹

Mmoja katika Ahlus Sunna aathirika na khutsba ya Sheikh Mughuniyah:

Ameandika Al-Allamah al-Kabir Sheikh Muhammad Jawad Mughuniyah (r.h), nanukuu: “Katika mwezi mtukufu wa Ramadhani mwaka 1387 A.H nilikuwa Baharain na ilikuwa ni wajibu wangu kupanda mimbari kila usiku kwa kusoma masaibu ya watukufu, katika usiku mmoja nilipanda mimbari na kabla ya kuanza kuongea nilisikia sauti inasema: “*Salamullahi alayka ya Husein Wala'nallahu Man Qatalaka*” Na maudhui ambayo nilikusudia kuyazungumzia yalikuwa hayahusiani na Imam Husein kabisa. Ghafila ikawa nimesahau maudhui na nikaanza kufasiri neno Husein (as) na Yazid, na kwamba yana maana gani kwa Shia.

Na kati ya yale niliyoyasema ni kwamba: “Neno Husein (as) mwanzo lilikuwa ni jina la Husein bin Ali (as), kisha likakua zaidi kadri muda ulivyopita likawa kwa wafuasi wake na wafuasi wa baba yake ni alama ya ushujaa na jihadi kwa ajili ya kumkomboa mwanadamu kutokana na dhulma na ukandamizaji, kielelezo cha kujitolea na kujitoa muhang kwa wanaume, wanawake na watoto kwa ajili ya kuhuisha dini ya Muhammad bin Abdillahi. Ama Yazid kabla ya Uislamu lilikuwa ni jina la mtoto wa Muawiya, ama leo hii kwa Shia ni alama ya ufisadi na ukandamizaji, uvunjifu wa heshima na udhalili, kisha ni mahala pa shari na ufisadi. Karbalaa

¹¹ *Qaswas Wakhawatir* Uk: 553

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

leo kwa Shia ni Palestina iliyotekwa na vilima vya Jaulan vya Syria. Ama watoto wa Husein na mateka wa kike wa Husein (a.s.), wao leo ni wanawake na watoto waliofukuzwa kutoka katika majumba yao, mashahidi wa Karbalaa ni wale waliouwawa kwa ajili ya kutetea haki ya nchi yao.” Al-Allamah anaongezea: “Niliposhuka tu, juu ya mimbari akanijia kijana na akasema: Huu ndio ukweli na hivi ndivyo inapasa kuufahamu Uislam na historia ya Kiislam, hususani tukio la Karbalaa. Kisha akaniuliza swalii na nikapata taufiki ya kulijibu ingawa sikuwa najua jibu lake kabla ya hapo, na walipomtambulisha kwangu nikajua kuwa yeye ni kutoka katika Suni wa Baharain na kwamba ana cheo kikubwa serikalini na ameathirika kutokana na maneno ya Al-Allamah athari kubwa kabisa.”¹²

Maelezo:

Hapana shaka kwamba mfano wa misimamo hiyo ambayo wanaathirika kwayo vijana wasiokuwa Shia mionganii mwa ndugu zetu wa Kisunni kutokana na majlisi za Huseni (a.s.) hususan katika kumi la mwazo la mwezi wa Muhamarram, ni kati ya faida kubwa ya uongofu na mafunzo, bali wameshaongoka wengi kati yao kwa baraka ya majlisi hizi. Mimi binafsi nimewaona wengi kati yao ambaa wameshakuwa wafuasi na wapenzi wakubwa wa Ahlul-Bait (as).

As-Sheikh Al-A’dham anahimiza majlisi za Imam Husein (as):

Al-Marja’ a mkubwa wa kidini Sheikh Murtadha Al-Answary (r.h) licha ya kwamba yeye ni mmoja kati ya maulamaa wakuu wa umma na mmoja wa wasimamizi wakuu wa Hawzah, lakini alitoka katika Haram ya Imam

¹² *Ashiatu Fil-Mizan* Uk. 454

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Husein (as) akiwa kazungukwa na wanafunzi wake miongoni mwa maula-maa na walimu wa Hawza ya Karbalaa tukufu, akawaambia: Twendeni tukasikilize mawaidha ya Sheikh Ja'far Shushtar katika majlisi yake mahsus ni tufaidike naye kwani nyoyo zetu aghlabu zinaelemea kwenye ugumu.¹³

Na Sheikh Al-Answary alikuwa anataka kuwafundisha wanafunzi wake kupenda majlisi za Husein (as) na kuwakumbusha kwamba mwanachuoni, mwanafunzi na mwalimu, wote wanahitaji kukumbushwa na kulelewa kiroho, na kudumu katika hilo, na moja ya vyanzo vya kufikia lengo hilo ni majlisi za Imam Hisein (as).

Taasisi za Husein (as) zilitoa watu kama hawa:

Moja ya sifa za makhatibu wa Huseiniyah ni kulia, Sheikh Ahmadi Al-Kafiy (r.h) anajulikana kwa mapenzi yake makubwa kwa Ahlul-Bait (as), hususan kwa Sayid Shuhadaa Al-Imam Al-Madhlum Al-Husein bin Ali bin Abi Talib (as). Mwalimu wake Hujjatul-Islam Sayid Muumin Zadeh anasema: Nilipokuwa nafundisha katika shule ya raia katika mji wa Mashhad, kati ya wanafunzi wa shule ya msingi alikuwa ni Sheikh Al-Kafiy akiwa katika siku za utoto wake.

Wanafunzi walipokuwa wanatoka wakati wa mapumziko na kucheza, mtoto huyu yaani Sheikh Al-Kafiy alikuwa anakuja kwangu na kunipa riiali mbili yaani fedha ya Kiarani na anasema: Nisomee mashairi ya masaibu ya Imam Husein (as). Na mimi namsomea, naye analia kwa uchungu mkubwa kana kwamba tumefanya majlisi ndogo ya Imam Husein (as), wakati huo alikuwa bado hajafikisha umri wa miaka kumi na tano, hadi akawa mashuhuri kwa sauti yake yenye kuhuzunisha kwa kusoma kwake Dua ya Kumail katika mikesha ya siku za Ijumaa katika Haram ya Imam Ridhaa (as).¹⁴

¹³ Yeki Swad Dastan Khawanadaniy, cha Kifursi Uk. 55.

¹⁴ Qaswas Wakhawatir Uk: 424

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

**Dondoo kutoka katika kaswida ya malenga wa Ahlul-Bait (as),
Ustadhi Abdul-Aziz Al-Andaliyb:**

Katika kumuomboleza Ayatullah Al-Udhmaa Al-Imam Muhamad Al-Husein Ashiraziy (r.h), anasema:

Simama tuzungumze juu ya Imam aliyeondoka, kwa kumsifu na kumtukuza, yule mwenye nafasi kubwa yenye mema mengi, yule mzuri mwenye fahari ya juu, faqihimkubwa wa pekee katika jithada na jihadi, mjuzi mwenye kufahamu fasihi, mtunzi mahiri, ameambatanisha fadhila na tabia njema, alama ya Mwenyezi Mungu kwa viumbe, Shiraziy Marja'a taqlid, ametumia umri katika kusoma, kusomesha na utafiti wenyewe manufaa kwa utunzi wake mwiningi ambapo amepewa taufiq na usawa, kwa mfano tu yatosha 'Enklopedia ya Fiqhi' kwa njia yake nzuri na ya kipekee katika nyanja zote. Ni mwenye jithada kwa kazi yake njema, kwa wepesi Magharibi na Mashariki ana miradi mingi, ni mwiningi wa jihadi amethibitisha ushujaa, hakuwa mwoga mwenye hofu, kwetu alikuwa chem-chem ya elimu na fadhila, mwenye msaada kwa kila jema na zuri, hakika sijaona wala sitoona mwenye kauli ya sawa na lengo. Kama utakuwa umeghibu mbali nasi ewe Abu Ridhwa na kila kilicho hai kitakufa, basi athari yako itabaki kwetu kuwa kumbukumbu bora. Hongera kwa kupumzika katika makazi ya kudumu. (Shawwal 1422 A.H.).

FAIDA YA TANO

Kukidhi haja na kutatua matatizo:

Anasema Mwenyezi Mungu (swt): "**Enyi mlionamini mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kumfikia. Na piganeni jihadi katika njia yake ili mpate kufaulu.**" (Sura al-Maidah: 35).

Hakika majlisi za Imam Husein (as) zinazingatiwa kuwa ni alama kati ya alama za kurejea kwa Mwewnyezi Mungu na kutawasali kwake na ni chan-

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

zo cha msingi cha kutatua matatizo ya kimaada na kiroho katika jamii yenyе maingiliano ya kimahusiano.

Katika mwisho wa karne ya kumi na nane na mwanzo wa karne ya kumi na tisa imejitokeza fikra inayoshambulia ulimwengu, muhtasari wake ni kwamba: "Hakika sisi hatuamini isipouwa fikra ya mada yenyе kukubali majoribio na kila kinachofungamana na yasiyoonekana ni jambo lisiloaminika wala kusadikika."

Kwa masikitiko makubwa wanaoathirika kwa fikra hii isiyotokana na Qur'ani na isiyokuwa ya Kiislamu ni idadi kubwa ya wananchi wa Kiislam isipokuwa wale tu waliohifadhiwa na Mwenyezi Mungu.

Lakini kadri muda unavyopita kumekuwa na haja ya kurejea kwenye kanuni za Mwenyezi Mungu za ghaibu na kuziamini mfano dua, tawasul na kuomba haja, na hayo ni kati ya mambo yanayotokana na itikadi yetu, Qur'ani imetilia mkazo jambo hili katika sehemu zake nyingi na sira ya Nabii na maasumina (as) vile vile imlisitsiza hilo, kama ambavyo wataalam wa kimagharib wameanza kutia mkazo kwamba kurejea kwa Mwenyezi Mungu na kuamini ghaibu kuna athari kubwa katika maisha ya mwanadamu, na kuna hali nyingi za maradhi ambazo zimeponywa hawezekani kuzithibitisha katika kanuni za kimaada, na kuna matatizo yametatuliwa kwa njia inayofanana na miujiza hatuwezi kuyahesabu wala kuyapima kimaada, sasa hayo tutayafasiri namna gani?

Mtaalamu wa kimagharibi anatia mkazo kwamba nguvu za ghaibu zinaathiri:

Mwandishi wa kitabu "Al-Insaanu Dhalikal-Majuhul" amejibu kwa kusema: Watu wameitakidi katika kila zama na kila sehemu kuwa kuna aina ya tiba ya haraka ya maradhi katika sehemu za miskitini, makanisani na katika sehemu takatifu. Lakini baada ya karne ya kumi na tisa itikadi hii imedhoofika kwa sababu watu wamevutika kwenye uvumbuzi na ugunduzi, ila ushahidi tulionao unawajibisha kupatikana jambo hili, kwa sababu kuna

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

ushahidi ambao haiwezekani kuufasiri kimaada. (Anatoa mfano anasema): Maradhi mengi yanategemea ripoti, mfano tibii ya mifupa, vidonda vyatumbo, kansa ya ngozi, saratani n.k. Wenye magonjwa hayo wamepona kwa njia ya dua na kutegemea ulimwengu wa ghaibu.

Haya ni mionganoni mwa mambo ambayo ameyasisitiza mmoja wa wataalamu mashuhuri wa kimagharibi kwa kusema: “Katika mapenzi yake (as) kuna miujiza ya ponyo kutokana na maradhi ya kiroho, na katika turba yake kuna ponyo kutokana na maradhi ya dhahiri, bali majlisi za Husein (as) vilevile ni sehemu ya kutatua matatizo mengi ya kijamii na kitabia” na haya ndio tutakayo yafafanua katika matukio yafuatayo:

Jicho lake lilipona kwa ajili ya kumlilia Husein (as):

Swalehe alikutana na Muhammad Rahim Ismail Biyka na alikuwa ni mashuhuri kwa kutawasali kwake kwa Ahlul-Bait wa Nabii (saww) na mapenzi yake ya moyoni kwa Sayid Shuhadaa (as). Na alishapata katika mlango huu rehema na baraka ya dhahiri na ya kiroho amenukuu kisa kilichomtokea akasema:

“Umri wangu ulikuwa miaka sita nilipopata maumivu ya jicho na nilibaki hivyo kwa muda wa miaka mitatu ndipo nikawa kipofu wa macho yote mawili. Na katika siku za Ashura majlisi ya maombolezo ya Husein yali-fanyika katika nyumba ya mjomba wangu mkubwa Al-Haji Muhammad Ismail Biyka na hali ya hewa ilikuwa ni ya jua kali, hivyo walikuwa wana-toa vinywaji baridi kwa waliohudhuria, nikamuomba mjomba wangu aniruhusu kuwapa vinywaji waliohudhuria. Akaniambia wewe ni kipofu hutawenza hilo. Nikamwambia nipe mtu wa kunisaidia. Akaafiki hilo na nikaanza kugawa vinywaji kwa waliohudhuria kwa msaada wake yeye.

Wakati huo huo Mu’inu Shari’ a Al-Istibahanatiy akawa amepanda mimbari na nikaanza kusoma masaiibu ya Bibi Zainab binti Ali (as), nikaathirika sana na nikalia hadi nikapoteza fahamu, ndipo nikamuona Bibi Zainabu (as) dada wa Imam Husein (as) akaweka mkono wake juu ya macho yangu

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

mawili na akasema umeshapona na maumivu yako yamekwisha. Nikafungua macho yangu nikakuta watu wa majlisi wamenizunguka kwa furaha na sururi nikamkimbilia mjomba wangu, waliohudhuria wakanikusanyikia, mjomba akanichukua hadi chumbani na akawatawanya watu pembezoni mwangu.¹⁵

Mfaransa amefanya majlisi ya maombolezo ya Husein (as):

Sheikh Muhammad Hasan Al-Maulawiy Al-Qandahariy amenekuu kwa kusema: Miaka hamsini kabla ya sasa nilikuwepo katika usiku wa kumi na nne wa Muharram katika nyumba ya kiongozi wa Muasasatu Maqaam Al-Imam Ridhaa (as) wa huko Mashhad tukufu, Sheikh Muhammad Baqir Al-Waidh, alisimulia kisa kwa kusema: Nilikuwa nimealikwa katika Muharram na wafanyabiashara wa Kiirani wanaoishi Paris kwa ajili ya maadhimisho ya msiba wa Husein (a.s.), nami nilikwenda huko, na katika usiku wa kwanza alikuja Mfaransa muuza vito vya thamani pamoja na mke wake na mtoto wake katika sehemu ile na akawaambia tafadhalini: Nilikuwa nimeweka nadhiri kufanya maombolezo ya Husein kwa muda wa siku kumi na nawaombeni mumtume Sheikh ambaye anasoma kwenu maombolezo haya aje anisomee msiba wa Imam Husein (a.s.) kwa muda wa siku kumi.

Waliohudhuria wakaniruhusu basi nikakubali. Nikasoma majlisi huko na wakazi wakafaidika na majlisi na wakalia humo. Mfaransa, mke wake na mtoto wake walikuwa wanasikiliza majlisi kwa lugha ya Kifursi, pamoja na kutokujua kwao lugha hiyo lakini ilidhihiri kwao huzuni na majonzi hadi siku ya tisa.

Nilipomaliza kusoma akanipa Lera mia moja nikakataa na nikamwambia sikubali hadi unieleze sababu ya nadhiri yako, akasema: "Katika mwezi wa Muharram mwaka uliopita nilipokuwa Bombei mwizi aliiba sanduku langu la vito vya thamani ambapo humo kulikuwa na mtaji wangu wote,

¹⁵ *Al-Qisas al-Ajibah* cha Sayid Dastaghiyb Uk: 42

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

nilikaribia kufa kwa huzuni na nikahofia kupatwa na ugonjwa wa moyo, chini ya chumba changu kulikuwa na barabara pana wanapita Waislam wakiwa bila ya viatu wakipiga vifua vyao na wanajipiga kwa zanjiri, nikashuka kutoka katika chumba changu na nikaingia kati yao na nikashirikiana nao katika maombolezo. Nikaweka ahadi katika nafsi yangu kuwa kama mwenye kuombolezwa atanirudishia vito vyangu nya thamani vilivyoibwa basi mwaka ujao nitalipa lera mia moja kwa ajili ya kufanya majlisi ya maombolezo popote nitakapokuwa. Na sikwenda hatua nydingi akanijia mtu akihema na akanipa sanduku na akaondoka. Nikafurahi sana nikaenda pamoja nao hatua chache kisha nikarejea chumbani kwangu na nikafungua sanduku na nikahesabu vito vyangu nya thamani nikakuta viko kamili hakikupungua chochote.”¹⁶

Maelezo:

Haifichikani kwa wenye akili ikiwa Imam (as) uangalizi wake na ukarimu wake unawajumuisha hata wasiokuwa Waislam sasa itakuwaje kwa wafiasi na wenye kumpenda? Hata kundi la baniani humshirikisha Bwana wa Mashahidi (as) katika faida za mashirika yao na huwapa Shia hisa yake ili kufanya maadhimisho ya maombolezo ya miezi ya Muharram na Swafar na hivyo wao hubarikiwa katika faida zao.

Arejeshewa nyumba yake iliyoporwa:

Mwanachuoni mchamungu na khatibu hodari wa mimbari ya Husein (a.s.) na mwandishi mwerevu Ayatullah Sayid Muhammad Kadhim Al-Qazuwiniy alikuwa ni kati ya mashujaa wa makhatibu wa mimbari ya Huseini (a.s.). Mmoja wa jamaa zake wa karibu ananukuu kutoka kwa Sayid Al-Qazuwiniy, anasema: “Alinijia – yaani Sayid Al-Qazuwiny - mmoja wa waumini akishitakia jirani yake kwamba amenyang’anywa nyumba, na akasema hakika yeye – yaani mnyang’anyi – ni kati ya wasik-

¹⁶ *Al-Qisas al-Ajiyah* cha Sayid Dastaghiyb Uk: 408.

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

ilizaji wa majlisi katika mimbari yako, nakuomba uzungumzie juu ya maudhui yatakayoitikisa dhamira yake ili arejee katika njia ya sawa.

Mimi nilizungumza juu ya mimbari kuhusu dhalma na hatima ya madhalimu, wanaokula mali ya haram na wanaopora haki za watu, na kutaja yanayowangojea wanyang'anyi mionganini mwa adhabu chungu Siku ya Kiyama. Siku ya pili mlalamikaji akarejea na kusema: "Mungu akulipe malipo mema, yule mtu ameathirika kutokana na maneno yako na amenirejeshea nyumba yangu siku ile ile."

Anaongeza Sayid Al-Qazuwiry, anasema: "Maneno yangu (juu ya mimbari ya Husein) yana athari hii ya haraka katika kutatua matatizo ya watu, haki-ka jukumu la kidini linaniwajibisha kutoa juhud zangu zote katika njia hii."¹⁷

FAIDA YA SITA

Mafungamano na mapenzi ya kina:

Anasema Mwenyezi Mungu (swt): "**Na mwenye kutukuza alama za Mwenyezi Mungu basi hilo ni katika uchamungu wa nyoyo.**" (Sura al-Hajji: 32).

Hakika kila sifa mionganini mwa sifa za moyo lazima iakisi katika vitendo na silka ya nje ya mwanadamu ambayo ndio hufichua sifa hiyo. Sifa ya kumwamini Mwenyezi Mungu hujiakisi kwa kumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kufanya ibada, amali na matendo mbalimbali katika maisha. Vivyo hivyo mapenzi ya mwislamu na mfuasi wa Ahlul-Bait (as) ni wajibu

¹⁷ *Qisasu Wal-khawatir* cha Sheikh Abdul - Adhim al-Muhtadiy Uk: 732.

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

yawe na utendaji na uhalisia unaofungamana na dhahiri ya maisha yake na nyenendo zake kufuatana na aya iliyotangulia, kwani hakika kutukuza alama inachukuliwa kuwa ni alama kati ya alama za uchamungu, na kati ya alama hizo muhimu zaidi ni kuhuisha utajo wa Ahlul-Bait (as), kuwapenda na kuwafuata kwa kutekeleza Aya: **“Sema siwaombi malipo ye yote kwaye isipokuwa kuwapanda jamaa zangu wa karibu.”** (Sura Shura: 23).

Kabla ya miaka 1300 A.H jamii ya Kiislam ilikuwa inaelewa vizuri uzito wa Ahlul-Bait (as) baina ya Waislamu, na ilikuwa inajua nafasi ya Husein (as) kwa babu yake (saww), kwa kufahamu hadithi sahihi ambazo zime-pokewa kuhusu jambo lake na kwamba yeye ni bwana wa vijana wa watu wa Peponi na ni Imam anayepaswa kutiiwa. Lakini vilipokuja vita vya siku ya kumi katika mwezi wa Muharram mwaka wa sitini na tatu hijiria, pazia likafunguka na majani ambayo watu wengi walikuwa wamejisitiri nayo yakapukutika mionganoni mwa wale waliokuwa wanadai ufuasi kwa Ahlul-Baiti (as) na kwa Husein (as). Kati yao kuna aliyebeba dhambi na akampiga vita Husein (as) na Ahlul-Bait wake, na mionganoni mwao kuna aliyefasiri kwa vitendo ufuasi wake na mafungamano yake ya kweli kwa Husein (as) na wafuasi wake, akajitokeza mbele ya maadui na akathibitisha mapenzi yake kwa damu kabla ya maneno.

Hivyo kinachotakiwa kwetu sasa si kingine isipokuwa ni kujitoa muhanga kwa damu kwa namna ambayo tutathibitisha ufuasi na utii, na pia kujunga, kuhudhuria, kuwahudhurisha wengine, na kufanya majlisi za nyumbani pia kuzishajiisha ili ziwe bora kadri iwezekanavyo na kuwa ni alama kati ya alama za usadikishaji, bayi'a na mapenzi kwa Husein (as).

Mwezi wa Muharram na minasaba mingineyo inadhihirisha mapenzi na imani kwa Ahlul-Bait (as), na inabainisha kiwango cha utoaji wako, ufuasi wako na msimamo wako, vinginevyo madai pekee hayatoshi abadani. Kwani sote tumefungamana na mapenzi ya Husein (as) lakini mafungamano haya, ufuasi na mapenzi yanatofautiana kati ya mtu na mtu

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

mwingine. Je anayeshiriki kwa ushirikiano baridi ni sawa na yule anayetoa mali, ni sawa na yule anayechangia kuanzisha majlisi, ni sawa na anayefanya majlisi za Huseini (a.s) majumbani?

Imepokewa kutoka kwa Abu Dhar al-Ghafarriy amesema: “Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anambusu Hasan na Husein (as) naye anasema: ‘Mwenye kumpenda Hasan na Husein (as) na kizazi chao kwa ikhilasi moto hautaunguza uso wake.’”¹⁸

Amenukuu al-Allamah Sayid Muhammad Ridhwaa as-Shiraziy mtoto wa Imam Shiraziy kisa hiki: “Mtu mmoja alikuwa katika mji na mtoto wake yuko katika mji mwingine pamoja na familia yake, siku moja asubuhi ali-wasiliana kwa simu na mzazi wake akisema: Hakika mimi usiku wa jana nimeona katika ndoto ambapo nimemuona Imam Husein (as) akiwa na nuru, utukufu na haiba isiyoelezeka, na pembezoni mwake kuna kundi ambalo nyuso zao zina nuru na athari za utukufu na utulivu, nikauliza: Hawa ni nani? Nikaambiwa: Hawa ni wanaompenda Husein (as).” Akasema: “Nikawa nakutafuta lakini sijakupata (kwa sababu mzazi wake alikuwa na mafungamano na Imam Husein (as) kwa muda wa miaka the-lathini mfululizo ambapo alikuwa na ada ya kusoma ziara ya Ashura kila siku nyumbani kwake). Nikauliza baba yangu yuko wapi? Mimi simuoni naye ni kati ya wanaompenda Imam Husein (as)? Wakasema: Hakika yeze amekata mafungamano yake na sisi. Lakini atarejea.

Al-Allamah Sayid Muhammad Ridhwaa as-Shiraziy anasema: Nikauliza: Vipi jambo hili? Mzazi wake akajibu: “Hakika ni ndoto ya kweli, mimi kabla ya masiku - kutohana na kushughulika kwangu na baadhi ya mambo - nimeacha kusoma ziara, lakini kuanzia sasa nitaanza kuisoma.”

¹⁸ Biharul-Anwar Juz: 43 Uk: 269 kutoka katika Kamiluz-Ziyaraat

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Aruzukiwa kutokana na mafungamano yake na Husein (as):

Katika khutba aliyoitoa Al-Marja'a Al-Alaa Ayatullah Al-Udhamaa Sayid Muhammad Shirazy (r.h) katika mji wa Qum mwaka 1414 A.H tumenukuu kisa hiki kutoka katika maneno yake: "Kulikuwa na khatibu mmoja, kwa kusema kwake tu juu ya mimbari: "*Swalla llahu Alayka ya Aba Abdillahil-Husein*" wahudhuriaji walikuwa wanabubujikwa na machozi na wanalia kwa sauti ya juu bila ya hiyari. Siku moja wakamuuliza: "Nini sababu kwa wengine pamoja na kurefusha kwao kisomo na kuongezea mashairi na visa wanashidwa kuwaliza wasikilizaji wakati ambapo wewe unawaliza kwa kusema tu "*Swalla llahu Alayka ya Aba Abdillahil-Husein*"?

Akasema: "Hakika mimi nina kisa cha ajabu kilinitokea katika mji wa Kashan, nayo ni kwamba usiku mmoja nilikuwa nimetoka katika majlisi ya mwisho niliyoisoma juu ya masaibu ya Imam Husein (as), na ilikuwa ni usiku sana na nilikuwa nimechoka sana kutokana na wingi wa majlisi katika usiku huo. Wakati nakwenda nyumbani njiani alinijia mtu mmoja na akaniomba niende kwake na kumsomea majlisi, alipokataa kukinaika na udhuru wangu nilikwenda pamoja naye, licha ya kuchoka kwangu sana, tukaingia nyumbani kwake. Akaniingiza katika chumba kisichokuwa na watu na kuta zake zimepambwa kwa vitambaa vyeusi na alama za maombiezo, katika kona moja kulikuwa na kiti kidogo yule mtu akaniambaia: Tafadhalii kaa juu ya kiti na usome masaibu ya Abu Abdillahil-Husein (as).

Nikamwambia nitamsomea nani! Na hakuna yejote kwako anayenisikiliza? Akasema: Msomee Bibi Fatma Zahraa (as). Nilipoanza kusoma: "*Swalla llahu Alayka ya Aba Abdillahil-Husein*" basi sauti za juu na vilio vya wanawake vikasika vikilia kwa uchungu sana pembezoni mwangu hali

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

mimi siwaoni. Hali yangu ikabadilika na nikaathirika sana nikateremka kwenye kiti na yule mtu akanipa fedha na nikaelekea nyumbani kwangu, nilipolala nikaona katika njozi mtu anayesema: "Hakika Bibi Fatma Zahraa (as) alikuwa katika majlisi hiyo akisikiliza kisomo chako kwa ajili ya mtoto wake Al-Husein Shahidi (as), na malipo yetu kwako kwa kisomo chako ni kwamba sisi tutajaalia athari kubwa katika neno lako "*Swalla llahu Alayka ya Aba Abdillahil-Husein*". Hivyo tangu siku hiyo ninaposoma sentensi hii hali ya wasikilizaji inabadilika na wanalia sana."¹⁹

Kati ya visa vizuri vyatujitolea na kufungamana na Imam Husein (as):

Amenukuu Sheikh Al-Adiyb Al-Hindiy (r.h) na alikuwa mwanachuoni mkweli kati ya wanachuoni watukufu wa India, ni maarufu na ni mashuhuri kwa wengi kati ya wenye elimu na uchamungu, amefariki kabla ya miezi michache katika mwaka wa 1421 A.H, alisema: "Kabla ya miaka 120 takriban (1300 A.H) kulikuwa na kijiji kimoja huko India ambacho humo kulikuwa na familia ambayo ni hiyo pekee ndio ilikuwa ikiwafuata Ahlul-Bait (Shia) kati ya familia zote zilizokuwa zinaishi humo, na ilikuwa na watu watatu mama, baba na mtoto wao kijana wa pekee.

Familia hii mwaka mzima walikuwa wanatenga kutoka katika pato lao la kila mwezi kifungu cha kufanya majlisi ya maombolezo ya Imam Husein (as) katika siku kumi za Muharram katika nyumba yao, na walikuwa wakiwaalika watu wote wa kijiji na vijiji vya jirani, majlisi ilikuwa inaendelea katika kila mwaka. Maadui wa haki na maadui wa Mwenyezi Mungu wakahisi hatari ya majlisi hii na wakaanza kuibana familia hii hadi wakafikia uamuzi wa kuwaangamiza wao na majlisi yao, wakaifanya nyumba njama ya shari karibu na mwezi wa Muharram. Fursa ilipopatikana na familia hiyo ya Kishia ilipokuwa nje, waovu hao waliin-

¹⁹ *Qisasu Wal-khawatir* Uk: 621 chapa ya Beirut

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

gia ndani ya nyumba na wakaiba kile kilichokuwemo ndani, hawakutosheka na hilo bali wakachoma nyumba yote na hakikubaki isipokuwa nguzo na baadhi ya kuta.

Familia hiyo ikajua jambo hilo na wakajaribu kujenga nyumba kadri walivyoweza, na nia yao ya kuikarabati nyumba haikuwa kubwa zaidi kuliko nia yao ya kukusanya kiasi cha fedha kwa ajili ya kufanya majlisi ya maombolezo ya Imam Husein (as), hususan ndani ya mwezi wa Muhamarram ambao ulikuwa umeshaingia. Wakafikiria njia mbalimbali za kupata mali na zote zilikuwa zimefungwa, hadi ikafikia mzazi wa kiume akafikiria njia moja lakini ilikuwa ngumu mno na akamweleza mke wake juu ya hilo, nayo ni kwamba “Tumuuze mtoto wetu wa pekee na tufanye majlisi kwa ajili ya Imam Husein (as).” Mama akachanganyikiwa sana lakini baba akanusuru msimamo huo kwa kumweleza mke wake: “Hakika mtoto wetu sio mtukufu zaidi kuliko watoto wa Husein (as), na Imam alijitolea kwa kila alichomiliki, na bila ya njia hii hatutaweza kufanya majlisi ya maombolezo na wakati ni kama unavyoona ni mfinyu sana.” Mama na mtoto wakakubali kujitolea huku.

Baba akamwambia mtoto muage mama yako kuagana kwa mwisho, wakakumbatiana na wakalia kilio cha uchungu sana, kisha walikwenda katika soko la watumwa na akaja mpanda farasi akamnunua mtoto na aka-toa fedha kwa baba na mtoto akaondoka pamoja naye.

Mtoto anaongeza kwa kusema: “Baada ya muda nilipokuwa natembea nyuma ya huyu mtu aliyepanda farasi tulikutana na mtu ana alama ya watu wema kana kwamba ni mtu mgeni, alikuja kwetu moja kwa moja na akamwambia huyo mpanda farasi: ‘Umemnunua kiasi gani huyu mtu (kijana)?’ Mpanda farasi akasema: ‘Umejuaje kwamba huyu ni mtumwa wangu? Na mimi kwa hakika sitaki kumuuzu.’ Akasema vyovyote iwavyo mimi najua kuwa ni mtumwa wako na mimi nitatoa kiasi kikubwa cha fedha. Mpanda farasi akakubali akachukua fedha na akanikabidhi kwa huyu mtu mgeni.

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

Mtoto anasema: Huyu mtu mgeni akawa ananiuliza wewe ni nani, mama yako ni nani, baba yako yuko wapi? Familia yako iko wapi na nchi yako iko wapi? Nikaanza kumweleza huyu mtu mwema kisa kamili, nilipomaliiza tu kueleza kisa changu nikajikuta niko katika kijiji changu kidogo na mbele ya nyumba yetu kisha akaniashiria: Ingia kwa wazazi wako kwa sababu wao bado wangali wanakulilia kwa kutengana nao na kwamba kurejea kwako ni malipo ya kufanya kwao majlisi ya maombolezo ya Imam Husein (as).

Sheikh Al-Adiyb Al-Hindiy anaongeza: Hakika kijiji hiki hivi sasa kimekuwa mji na watu wake wote wamekuwa ni wafuasi wa madhehebu ya Ahlul-Bait (as) kwa sababu ya kujitolea huku kukubwa kwa familia hii tukufu.²⁰

Maelezo:

Familia hii yenye taufiq imebeba majukumu ya kidini yaliyo juu ya mabega yake katika muongo huo katika zama iliyopita, na wametekeleza wajibu wao katika jambo muhimu kabisa la mustakabali katika historia ya Kiislamu, kwa kumnusuru mtoto wa binti ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), sasa ni zamu yetu sisi wafuasi wa Ahlul-Bait katika wakati huu ambao umuhimu wake ni mkubwa ambapo kuna harakati za fikra potovu mbalimbali zinazonyemelea madhehebu ya Ahlul-Bait kwa shari. Sasa sisi tunafanya nini? (wakati ni huu hujachelewa bado).

²⁰ Kutoka katika muhadhara wa al-Allamah Sayid Huseiniy Shiraziy mtoto wa Ayatullah al-Udhmaa Sayid Swaadiq Shiraziy

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

MWISHO

Husein ndio mshumaa wa nuru katika wakati wa giza la fikra potofu, hivyo kila mmoja wetu awashe mshumaa ili ajitengenezee mwanga katika maisha yake ya Duniani na kesho Akhera.

Hakika mwanzo – wa amali ye yeyote ya kheri - aghlabu hukabiliwa na aina mbalimbali za kusita sita, lakini pindi mwanadamu anapoanza huona tau-fiq ya Mwenyezi Mungu inamuunga mkono na kumhimiza kuendelea, kwa kweli jambo hili ni mujarabu.

Wale walioweka azima ya kuasi majlisi ya Huseini (a.s.) katika nyumba zao, wakaanza na wahudhuriaji wachache na uwezo mdogo, basi watabarikiwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Kuchelewa kuanza ni bora zaidi kuliko kutoanza kabisa. Hivyo wekeni azma na jueni kwamba wale walioanza kabla yenu hawakuwa wanamiliki mali nyingi kwa ajili ya hilo, bali ni kwa uwezo mdogo kisha baraka za Husein (a.s.) zikawashukia. Amesema Mwenyezi Mungu (swt): “**Na shindaneni katika kheri.**”

Wasalaam Alaykum Warahmatullahi Wabarakatuh

25 Shawwal 1422 A.H.

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba' Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekeea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume
Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia
iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali
87. Uislamu na dhana

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqlain
102. Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
114. Iduwa ya Kumayili.

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Idil Ghadiri
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

141. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu *Fiqhi al-Sunnah*
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt
(Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Kati ya Alama kuu za dini Swala ya Jamaa.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya Pili
161. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
162. Falsafa ya mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Huduma ya Afya katika Uislamu
164. Hukumu za Mgonjwa

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

165. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein
166. Uislamu Safi
167. Majlis ya Imam Husein
168. Mshumaa
169. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
170. Uislam wa Shia

Majlisi za Imam Husein (a.s) Majumbani

BACK COVER

Kitabu hiki kidogo kwa umbo lakini kwa hakika ni kikubwa kwa yale kili-choyabeba mionganoni mwa nasaha, mafunzo na mifano chungu nzima yenye kujaa mazingatio katika maisha yetu ya kila siku na yenye manufaa hapa duniani na kesho Akhera.

Kitabu hiki kinalenga sana kujenga maadili mema na tabia nzuri katika familia zetu na jamii yetu, hususan kwa kizazi chetu ambacho ndio kwanza kinainukia na kupambana na mambo ambayo yanashughulisha akili zao na fikra zao na kuwaweka mbali na utamaduni wao na mafunzo mema ya dini yao, ambapo nafasi imekuwa ni finyu kiasi kwamba mtu hana nafasi ya kuhudhuria vizuri katika madrasa. Hivyo, mwandishi wa kitabu hiki anahamasisha na kuraghibisha kuwepo majlisi ndogo katika ngazi ya familia, mtu na familia yake, jamaa zake na jirani zake na kufanya majlisi ndogo ambayo haihitaji gharama kubwa, lakini faida yake na malipo yake ni makubwa. Majlisi ambazo zitalea nafsi zetu, familia zetu, jamii yetu na vizazi vyetu malezi mazuri ya kidini, lakini pia yatasaidia kujenga na kuimarisha familia zetu na nyumba zetu na kuzipa ulinzi na kinga kutokana na maafa na balaa mbalimbali na kuwa ndio sababu ya sisi kuteremshiwa baraka na rehema za Mwenyezi Mungu.

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv-com

Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info